# Ugharimiaji wa elimu ya msingi Dar es Salaam
# Hali ya upatikanaji wa taarifa za shule ukoje?

## Matokeo muhimu

- Walimu wengi hawajui shule zao zinapaswa kupokea kiasi gani cha ruzuku ya elimu
- Mara nyingi ruzuku ya elimu inatolewa sehemu tu, na wakati wa kupatikana si wa uhakika
- Ni vigumu kupata taarifa za Serikali mashuleni kutokana na utunzaji mbaya wa kumbukumbu na hofu ya vitendo vya ulipaji kisasi

## Utangulizi

Tangu mwaka 2002, Serikali ya Tanzania imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ikiwa na madhumuni maalumu mawili: mosi, kupanua upatikanaji wa elimu ya msingi, na pili, kuinua viwango vya ubora wa elimu hiyo. Ili kufanikisha malengo haya, Serikali inapeleka fedha mashuleni kwa namna mbili:

a) Ruzuku ya elimu, inayotengwa kwa madhumuni ya matengenezo ya shule, kununua vifaa vya kujifunzia, na kuendesha mitihani ya shule; na
b) Fedha za maendeleo, zinazotengwa kwa madhumuni ya kukuza ubora wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vinavyohitajika mashuleni.

Muhtasari huu, ambao ni sehemu ya utafiti wa ufuatiliaji ulioendeshwa katika shule za msingi za Serikali 40 mkoani Dar es Salaam kati ya mwezi Agosti na Desemba mwaka 2010, unachunguza: kiwango cha uelewa wa walimu kuhusu kiasi cha ruzuku ya elimu ambacho shule yao inastahili kupokea; kuhusu wakati katika mwaka ambapo ruzuku ya elimu inapatikana; na kwa kiwango gani wananchi wanaweza kupata taarifa kuhusu ruzuku ya elimu.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba walimu wengi hawajui ni kiasi gani cha fedha ya ruzuku ya elimu shule zao zinastahili kupokea kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Local Government Authorities (LGAs*)). Pia, fedha zinazowafikia shuleni ni sehemu tu ya kiasi ambacho shule zao zinastahili kupokea. Mwisho, utafiti umebaini kwamba taarifa kuhusu kiasi cha fedha zinazopelekwa katika shule na matumizi yake ni taarifa ambazo wazazi na wananchi kwa jumla hawawezi kuzipata kwa urahisi.

Muhtasari huu unapendekeza kwamba taarifa kuhusu viwango vya ruzuku ya elimu viwekwe wazi kwa shule na wazazi katika mwanzo wa mwaka wa fedha, na kwamba ratiba ya kupeleka fedha hizo kwenye shule izingatiwe.

Muhtasari huu umeandaliwa chini ya uangalizi wa Rose Aiko wa Uwazi iliyopo Twaweza-HivosTanzania.

Uwazi, S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org
Umetolewa Mei, 2011.

## Jambo la 1: Walimu wengi wana uelewa mdogo kuhusu kiasi cha ruzuku ya elimu ambacho shule yao inastahili kupokea

Asilimia 80 ya walimu hawajui kiasi cha ruzuku ya elimu ambacho shule yao inastahili kupokea na ni wachache tu wanaweza kutaja kiasi kamili cha Dola za Marekani 10 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka. Kiasi kilichotajwa na walimu wakati wa utafiti huu ni pamoja na Shilingi 10,000, Shilingi 5,000, Shilingi 3,000, na Shilingi 1,000. Walimu wengi wameonesha kwamba ingawa fedha hizo zinapaswa kufika shuleni kwa mafungu katika kila robo mwaka, ratiba hiyo kamwe haizingatiwi.

Walimu hata hivyo wanaelewa vizuri kanuni ya kugawa fedha zinazopokelewa shuleni kwao kwa mafungu ili kugharimia matumizi mbalimbali, na kanuni hiyo inafuatwa kikamilifu. Lakini kwa kuwa mara nyingi shule zinapelekewa fedha nusu nusu au kwa kuchelewa, wakati mwingine walimu wanajikuta wameingia katika hali ya madeni kwa kuwa wananunua vifaa kwa matumizi ya darasani kwa mkopo.

Mathalani, mnamo mwezi Mei 2010 mgawo wa fedha kwa Shule ya Msingi Mapambano ulikuwa Shilingi 250,919.23. Kanuni ya mgawo wa ruzuku ya elimu kwa mafungu ya matumizi inaagiza kwamba fedha zinapofika shuleni zitumike kama ifuatavyo:

- asilimia 20 kwa matengenezo;
- asilimia 40 kwa ununuzi wa vitabu vya kiada na vitabu vya walimu;
- asilimia 20 kwa ununuzi wa chaki, peni, penseli na madaftari ya mazoezi;
- asilimia 10 kwa shughuli za utawala;
- asilimia 10 kwa ununuzi wa karatasi za mitihani na uchapishaji.

Kulingana na kanuni hii, mwalimu mkuu ana Shilingi 100,367 kwa ununuzi wa vitabu kwa shule yote yenye wanafunzi 810; Shilingi 25,091.92 kwa shughuli za utawala, ambazo kwa kawaida ni pamoja na usafiri kwenda katika ofisi za Serikali na safari nyingine za kikazi, kugharimia semina za walimu, na kadhalika; na Shilingi 50,183.85 kwa matengenezo mbalimbali. Ikizingatiwa kuwa kiasi hiki ni kidogo sana, unajiuliza kitaweza kukarabati madawati mangapi, vishikio vya milango vingapi, au vyoo vibovu vingapi.

**Kielelezo cha 1: Je, unajua ni kiasi gani cha ruzuku ya elimu shule yako inastahili kupokea katika mwaka 2010/11?**




**Chanzo cha takwimu:** Uwazi, 2010.

**Maoni ya walimu**

"Tunasubiri tu fedha hizo zifike, na kufika kwake pia mara nyingi ni muujiza," anasema mwalimu mkuu mmoja, ambaye maoni yake yanaakisi maoni yaliyokwishatolewa na walimu wengine wengi.

"Wakati mwingine tunawaomba wafanya biashara watupatie huduma kwa mkopo na fedha zinapofika tunalipa madeni hayo," anasema mwalimu mwingine.

## Jambo la 2: Taarifa kwa 'umma' hazipatikani kwa urahisi

Utafiti umechunguza taarifa zilizobandikwa wazi kwenye kuta za ofisi ya mwalimu mkuu katika shule nyingi zilizotafitiwa. Taarifa hizo zinaonesha takwimu kuhusu idadi ya wanafunzi na idadi ya mashimo ya vyoo katika shule, kumbukumbu za mapato ya shule na matumizi, na taarifa kuhusu mipango ya shule ya baadaye.

Ingawa taarifa hizi kimsingi zinapaswa kuwa wazi kwa wananchi, haikuwezekana kupata taarifa zozote bila maombi maalumu na kupata kibali kutoka "ngazi za juu". Watafiti walilazimika kupata idhini kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ambako barua iliyonakiliwa kwa wakurugenzi wote wa manispaa ilitolewa. Katika baadhi ya shule, idhini hii ilitosha kwa shule kutoa taarifa hizi za umma, lakini katika shule nyingine, ilikuwa lazima kupata barua nyingine iliyotiwa saini na Afisa Elimu wa Manispaa inayohusika.

Ufuatiliaji wa barua na vibali ulichukua majuma 6. Hata baada ya kuwasilisha vibali vyote vinavyohusika, baadhi ya walimu bado walihitaji kuhakikishiwa kuwa hawatahatarisha ajira zao au fursa zao kazini katika siku zijazo kwa kutoa taarifa zilizoombwa. Hali ya kuficha taarifa zinazopaswa kuwekwa wazi kwa umma ilionekana katika utoaji wa taarifa zinazohusu masuala ya shule, licha ya kuwepo sera na maagizo yanayoelekeza kinyume cha mwenendo huo.

## Jambo la 3: Uwekaji kumbukumbu kuhusu mtiririko wa rasilimali kwenye shule uko hafifu

Kutokana na utunzaji mbaya wa kumbukumbu katika shule, ni changamoto kubwa kuweza kuelewa mahesabu yanayotolewa katika ripoti za ruzuku ya elimu katika ngazi ya shule. Walimu waliulizwa kutoa taarifa ya kiasi cha ruzuku ya elimu iliyopokelewa shuleni kwao katika mwaka 2008, 2009, na katika robo ya kwanza ya 2010. Hata katika swali hili rahisi walimu walionesha kukanganyikiwa hali iliyolazimu kuliangalia suala hili kwa kina, na kwenda nje ya kumbukumbu za shule, kwa kuangalia malipo yanayofanywa na idara ya elimu ya kila manispaa.

Kulikuwa na mambo mengi ya kutatiza yaliyohusiana na kueleweka kwa taarifa zilizopatikana. Kwanza, walimu wakuu wengi waliohojiwa wanachukulia kuwa mwaka wa fedha unaanza mwezi Januari (yaani, sambamba na mwanzo wa mwaka wa masomo), wakati ambapo mwaka wa fedha wa Serikali unaanza mwezi Julai. Hata hivyo, malipo yakiwa yanafanyika katika kila robo mwaka, kinadharia bado inawezekana kutengeneza/kuandaa ripoti ya mahesabu ambayo yanalingana na malipo kutoka halmashauri za manispaa kwenda kwenye shule. Jambo hili halikuweza kufanyika kutokana na fedha kupokelewa shuleni kwa nyakati zisizoendana na ratiba ya mgawo (kila robo ya mwaka). Pili, katika shule nyingi, hakuna utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu/ taarifa za malipo na kuzitoa pale zinapohitajika. Katika baadhi ya shule, walimu walikuwa wakirejea kumbukumbu za mikutano ya kamati za shule ili kupata taarifa, badala ya kutumia kumbukumbu za mahesabu za shule. Katika hali mbaya zaidi, taarifa hazikuweza kupatikana kabisa kwa sababu kulikuwa na mabadiliko ya uongozi wa shule, na taarifa zinazohusika hazikukabidhiwa rasmi na mkuu wa shule aliyeondokwa kwa mkuu wa shule mpya.

## Hitimisho

Muhtasari huu unaonesha kwamba walimu wengi hawajui kiasi cha ruzuku ya elimu ambacho shule zao zinastahili kupata, kwamba mara nyingi fedha zinazopatikana hazitoshi, na pia hakuna uhakika fedha zitapatikana lini. Muhtasari huu unaonesha kuwa katika shule nyingi mfumo wa uwekaji kumbukumbu ni hafifu, na kwamba upatikanaji wa taarifa kuhusu rasilimali za shule umefanywa kuwa mgumu, na hivyo kusababisha wananchi kushindwa kupata taarifa muhimu.

Uwazi inapendekeza hatua tatu za kutatua changamoto hizi:

- Kiasi cha ruzuku ambacho shule zinastahili kupokea na ratiba za malipo zijulikane wazi kwa shule/walimu wakuu na wazazi mwanzoni mwa kila mwaka wa fedha wa Serikali. Itakuwa vema taarifa hizi zitolewe na Wizara ya Elimu mbele ya waandishi wa habari na zisambazwe kupitia vyombo vya habari na kwa njia nyingine zinazofaa;
- Iwe ni lazima kwa utawala wa shule kuweka kwa usahihi kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha zote zinazopelekwa mashuleni, na iwekwe mifumo ya kuhakikisha makabidhiano ya taarifa yanafanyika kwa umakini unaostahili kunapotokea mabadiliko katika uongozi wa shule; na
- Walimu wapewe mamlaka ya kutoa taarifa zinazopaswa kuwa wazi kwa umma kwa mtu yeyote anayehitaji taarifa hizo, bila kumtaka atoe sababu za kimaandishi kueleza kwa nini anataka kujua taarifa hizo.

**Kiambatisho: Shule za msingi za Serikali zilizotembelewa katika utafiti**

| Wilaya ya Temeke (16) | Wilaya ya Ilala (13) | Wilaya ya Kinondoni (11) |
|---|---|---|
| Vijibweni | Buguruni Moto Mpya | Kawe A |
| Mji Mwema | Boma | Kumbukumbu |
| Mivinjeni | Amana | Mapambano |
| Tua Ngoma | Buguruni Viziwi | Mbuyuni |
| Kibada | Msimbazi Mseto | Oysterbay |
| Chang'ombe | Gerezani | Kinondoni |
| Geza Ulole | Muhimbili | Msisiri |
| Mtoni Kijichi | Ukonga | Mlimani |
| Kimbiji | Buguruni Moto | Bunju A |
| Kurasini | Buguruni | Mtongani |
| Kibugumo | Mnazi Mmoja | Kunduchi |
| Tandika | Uhuru Wasichana | |
| Mgulani | Bunge | |
| Mikwambe | | |
| Kigamboni | | |
| Mbagala | | |

### Chanzo cha takwimu

Muhtasari huu ni sehemu ya ufuatiliaji wa wananchi unaoendelea kupitia Uwazi, www.uwazi.org. Takwimu zilikusanywa kupitia utafiti wa ufuatiliaji uliofanywa kati ya mwezi Agosti na Desemba 2010. Takwimu zote zinaweza kupatikana kutoka Uwazi.